# SHULE YA UPILI YA MARANDA

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

KITANGULIZI WA MWIGO 2022

102/3 KISWAHILI (FASIHI) Karatasi ya 3

Juni 2022 – Saa: 2½

Jina : ........................................................................ Nambari yaUsajili: ................

Mkondo: ........... Sahihi ya mtahiniwa: ............. Tarehe: ......../06/2022.

***Maagizo***

a) *Jibu maswali **manne** pekee.*
b) *Swali la **kwanza** ni la **lazima**.*
c) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: Riwaya, Fasihi Simulizi, Tamthilia na Hadithi Fupi.*
d) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
e) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
f) *Majibu yote sharti yaandikwe kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.*
g) *Karatasi hii ina kurasa **13** zilizopigwa chapa.*
h) *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*
i) *Andika nambari kwa maswali uliyoyajibu kwenye jedwali ulilochorewa hapo chini.*

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

## SEHEMU A: USHAIRI

### 1. Lazima

*Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

**Milingoti**

Wanakwenda... wanakwenda...
Wanapiga hatua labda!
Labda... labda... labda!
Mwendo wa dhana yao!
Wanakwenda kumbe wamesita.
Safari ya kuwepo na kutokuwepo!

Hatua zao kubwa: chapchap...
Miondoko sawa na jongoo
Wanakwenda pasi na kwenda
Safari ya dhana... pekee

Hatua zao kubwa na nia pia
Nia zin'otoka ndani kuishia ndani
Maishilio ni nafsi zao

Wanapiga hatua kubwa
ela wametwama!
Kisha:
kwa magondi husimama
pasi na nguvu huja kuima
kutaka kugusa mbingu.

Mara mojamoja hutazama chini,
kuchungua mbilikimo
na kuhakikisha,
jinsi walivyoziteka akili zao
kuzichezea, kuzisuguasugua
mchezo wenye manufaa kwao

Mara nyingine hutazama chini
kutemea mate mbilikimo
"Rasharasha ya marashi!"
Utawasikia wakisema;
Na
ajabu mbilikimo hufarijika!
Hivyo daima huendelea kwenda
Huku wamesimama milingoti

Kwa nadra hutokezea kusikia
Mmoja ameshateguka
        na kupoteza uzani
        kwa ule unene wao
Na kisha hulalama na kulani
        eti wameangushwa
na mbilikimo!

a) "Dhamira ya nafsneni ni kukashifu tabia za nafsinenwa," Thibitisha. (alama 5)

b) Changanua mtindo katika shairi hili. (alama 5)

c) Chambua muundo wa shairi hili. (alama 3)

d) Fafanua toni inayodhihirika katika shairi hili. (alama 2)

e) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. (alama 3)

## SEHEMU B: RIWAYA

A. Matei: *Chozi la Heri*

*Jibu swali la 2 au la 3.*

2. Jadili nafasi ya vijana katika kuiendeleza na kuiumba jamii kwa mujibu wa riwaya ya *Chozi la Heri.* (alama 20)

3. (a) Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali:

" Mawio ya leo yanaelekea kuwa na kiza kisicho cha kawaida," anajisemea kijakazi Sauna huku akijipindua kuusikiliza mlio wa king'ora unaosikika kwa mbali. Anaenda miayo na kujikokota kutoka kitandani. Maungo yake yanahisika kuwa mazito kama nanga. Anatamani kurudi kitandani alale lakini inabidi amtayarishie Bi. Kangara kiamshakinywa; ana miadi ya mapema na mzalendo mmoja jijini. Sauna anaingia jikoni na kujifunga kimori, tayari kuanza kuchoma mandazi. Mara moyo unaanza kumwenda mbio na vipapasio vya akili yake kusimama wima. Anajihisi kama anayetarajia kuanza kinyang'ayiro kikali cha upiganaji masumbwi. Kwa umbali anasikia mbisho hafifu langoni mwa jumba hili. Anatoka nje kwenda kuitikia mbisho huu. Ghafla, uso wake unakumbana ana kwa ana na polisi! Mara anasikia moyo wake ukimwambia, "Yako ya arubaini imefika," huku akijaribu kuvaa tabasamu na kuwakaribisha maafisa hawa nyumbani.

(i) Bainisha aina nne za taswira zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

(ii) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 6)

(b) Jadili ujumbe unaojitokeza katika masimulizi ya wahusika wafuatao:

i. Kaizari (alama 5)

ii. Chandachema (alama 5)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

P. Kea: Kigogo

*Jibu swali la 4 au 5*

4. "Mashujaa halisi ni wale waliouliwa msituni wakipigana. Waliwahangaisha wakoloni hata wakawatimua. Hao waliofungwa walitufaa vipi? Mtu anaweza kutoa mchango gani akiwa gerezani? Uhuru wa waliofungwa ulikuwa mikononi mwa waliokuwa vitani. Kama wangelaza damu ama kuzembea, wafungwa wangejifia huko korokoroni."

   (a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

   (b) Eleza mchango wa msemewa katika kujenga ploti ya tamthilia hii. (alama 5)

   (c) Onyesha jinsi mashujaa halisi walivyopigania ukombozi wa Sagamoyo. (alama 11)

5. "Umeugonga msumari kichwani nyanya, lakini wake nao wajirudi, wameenda sana! Vinginevyo asasi ya ndoa imo hatarini."

   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

   (b) Eleza vipengele **viwili** vya kimtindo vinavyojitokeza katika dondoo. (alama 2)

   (c) Kwa kurejelea tamthilia nzima, thibitisha kuwa asasi ya ndoa imo hatarini. (alama 14)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

*A. Chokocho na D. Kayanda (Wah.): Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 6 au 7*

6. (a) Eleza namna haki za watoto zinavyokiukwa katika hadithi ya "*Tulipokutana Tena*" (alama 10)

b) Huku ukitoa mifano mwafaka, eleza matumizi ya jazanda katika hadithi "*Shibe Inatumaliza*" (alama 10)

7. "Huwezi kushindwa na mtihani wa shule na vilevile <u>kushindwa na mtihani wa maisha</u>."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Eleza sifa **sita** wa msemaji wa maneno haya. (alama 6)

(c) Kwa kurejelea hadithi nzima ya *Mtihani wa Maisha*, onyesha jinsi msemewa anavyoshindwa na mtihani wa maisha. (alama 10)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. *Soma maigizo yafuatayo kisha ujibu maswali*

**MSAKATONGE:**
Limekucha sasa jua, nimetoka gizani,
Haki zangu nazijua, 'tasema nataka nini,
Mzigo huu najitua, siumbuki mwako kondeni,
Vifaa naweka chini, kazi leo nagomea.

**MWENYETONGE:**
Hayo unayoyanena, hapa hayatakikani,
Ni hatia kubwa sana, kabisa iso kifani,
Mambo yaso na maana, kayasikia na nani,
Vifaa kuweka chini, wajitosa taabani.

**MSAKATONGE:**
Malipo ninayopata, sio pesa ni mapeni,
Maisha yangu ni mwata, hayaniishi madeni,
Shida zinaniambata, kwa wangu umaskini,
Vifaa naweka chini, kazi leo nagomea.

Nitazame mwili wangu, sinayo siha mwilini,
Haitoshi kula yangu, kwa kuwa sina mapeni,
Ni mararu nguo zangu, nachekwa kiwa njiani,
Vifaa naweka chini, kazi leo nagomea.

**MWENYETONGE:**
Uchumi 'meharibika, kote kote duniani,
Hata huko Amerika, walia nifanye nini,
Kuache kulalamika, uchangamke kazini,
Vifaa kuweka chini, wajitosa taabani.

Utaweza kuushika, uvuvi dhiki majini?
Mararu kujifunika, si fedheha mwafulani,
Mradi wanufaika, na malipo hatimani,
Vifaa kuweka chini, wajitosa taabani.

**MSAKATONGE:** Kwa miaka na dahari, natumika kiwandani.
Silioni lenye heri, kwa nguvu za muilini,
Inaniandama shari, nyumbani hata kazini,
Vifaa naweka chini, kazi leo nagomea.

**MWENYETONGE:** Basi tuache hasira, isiongoze njiani,
Tuitumie busara, tuketi hizi thenini,
Bila hata ya papara, tupime kwenye mizani,
Vifaa kuweka chini, wajitosa taabani.

a) Bainisha kipera cha maigizo kinachorejelewa. Thibitisha jibu lako kwa mifano **mitatu**. (alama 4)

b) Eleza ujumbe wa maigizo uliyoyasoma hapo juu. (alama 4)

c) Eleza shughuli **tatu** za kiuchumi ambazo zimejitokeza katika utungo huu. (alama 3)

d) Wewe ni mwigizaji wa michezo jukwaani. Eleza mambo **matano** ambayo utazingatia katika uwasilishaji wako. (alama 5)

e) Unanuia kutumia mbinu ya kuchunza / utazamaji kukusanya habari kuhusu miviga ya tohara. Eleza manufaa **manne** ya kutumia mbinu hii. (alama 4)

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................

......................................................................................................................................